N14/2/ABSWA/SP1/SWA/TZ0/XX/T

88142319

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI B – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SWAHILI B – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI B – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Wednesday 12 November 2014 (morning)
Mercredi 12 novembre 2014 (matin)
Miércoles 12 de noviembre de 2014 (mañana)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for paper 1.
- Answer the questions in the question and answer booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.


© International Baccalaureate Organization 2014

https://xtremepape.rs/


Blank page
Page vierge
Página en blanco



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU A**

# EPHRAIM SEKELETI: MSANII MWENYE MAFANIKIO YA NYIMBO ZA INJILI ZAMBIA ANAYEIMBA KWA KISWAHILI



Nyota wa muziki wa Injili* wa nchini Zambia, Ephraim Sekeleti, ni kati ya waimbaji wa muziki huo wanaokubalika sana nchini Tanzania.

Ni mtunzi na muimbaji mzuri; uwezo wa kuimba baadhi ya nyimbo zake kwa lugha ya Kiswahili ni kati ya sifa zinazochangia umaarufu wake zaidi nchini.

Licha ya kufanya muziki wake nchini Zambia, amewahi kuja nchini Tanzania na kurekodi albamu yake nzima kwa lugha ya Kiswahili. Kati ya nyimbo zake zinazotamba hapa nchini ni pamoja na “Baraka Zako”, “Uniongoze” na “ Mwaka Huu”.

Ephraim hajui Kiswahili fasaha lakini nyimbo zake hizo alifundishwa kuziimba kwa lugha ya Kiswahili na mchungaji ambaye pia ni muimbaji wa nyimbo za Injili kutoka Tanzania, Ency Mwalukasa. Muimbaji huyo amesema ataendelea kuimba nyimbo za injili kwa sababu zimempa changamoto ambazo zimemfanya kuwa mtu wa nguvu zaidi.

Ephraim Sekeleti alizaliwa mwaka 1983 katika mji wa Kalulushi nchini Zambia. Alimaliza elimu yake ya sekondari katika shule ya Kalulushi mwaka 2001. Yeye ni mtoto wa pili kutoka mwisho kati ya watoto sita wa familia yao na aliingia kwenye muziki wa Injili tangu akiwa kinda. Alifundishwa kupiga kinanda na mmishionari alipokuwa bado mdogo.

Mwaka 2002 akiwa na kiu ya kurekodi albamu yake, aliamua kwenda Afrika Kusini kwa kutumia kiasi kidogo tu cha pesa alichokuwa nacho. Nia ilikuwa kurekodi albamu yake ya kwanza. Pamoja na jitihada hizo baada ya kufika nchini Afrika ya Kusini, alijikuta anarekodi nyimbo mbili tu kati ya albamu nzima.

Hivyo akaamua kujiingiza katika jukwaa la Pretoria na ndipo akapata fursa ya kuimba mbele ya Rais wa Afrika Kusini wakati huo, Nelson Mandela.

Karibu aamue kuacha kuendelea na muziki wa Injili ili aimbe muziki wa kidunia lakini akawa muaminifu kuendelea na uimbaji wa Injili. Mlango ulifunguka na kumruhusu kurekodi albamu ya kwanza iitwayo “Temba Baby”.

Baada ya kurekodi na kuuza nakala za kutosha za albamu hiyo ya “Temba Baby”, aliamua kurudi nyumbani kuwekeza fedha zake. Aliona awekeze zaidi kwenye albamu yake ya pili iliyopata mafanikio makubwa iliyoitwa “Limo Ndanaka”. Albamu hii ilifanya vizuri kwenye chati mbalimbali za muziki wa Injili. Anafurahi kuona nyimbo zake zikiwa na athari nzuri kwa watu.

Imetoholewa kutoka na mwandishi wetu wa *Nipashe* (2013)

* Injili: aina ya Muziki wa kidini




https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU B**

## SERIKALI: UHAMIAJI WA ANALOJIA KWENDA DIJITALI UFANYIKE KWA AWAMU

Mfumo wa mawasiliano Tanzania unabadilika kutoka mfumo mmoja (analojia) hadi mwingine (dijitali) ambao unafaa zaidi. Serikali imeitaka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuhakikisha kwamba zoezi la uhamiaji wa mfumo wa matangazo ya analojia kwenda dijitali unafanyika kwa awamu ili kuondoa hofu ya wananchi kukosa matangazo ifikapo Desemba 22 mwaka huu.



Agizo hilo limetolewa jana na Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Dkt. Fenella Mukangara, wakati akizungumza na baadhi ya viongozi wakuu wa TRCA, ambao waliwasilisha taarifa na mabadiliko ya mfumo huo ofisini mwake. Aidha, Waziri huyo aliusisitizia uongozi huo kuendelea kutoa elimu sahihi kwa umma kwa kuzingatia ratiba ya uzimaji wa mitambo hiyo iliyotolewa.

Mkurugenzi wa Utangazaji wa TRCA Habi Gunze akiwasilisha taarifa hiyo kwa Waziri alisema, uzimaji wa matangazo hayo utafanywa kwa awamu tano. Alisema kwa kanda ya Dar es Salam, mitambo ya analojia itazimwa Desemba 31, mwaka huu saa sita usiku na maeneo husika ni jiji la Dar es Salaam, Kibaha, Bagamoyo… Vituo vitakavyohusika ni TBC1, ITV, EATV na Capital TV. Vituo vingine vitakavyoathiriwa eneo la Dar es Salaam ni pamoja na Tumaini TV, ATN, Mlimani.

Katika kanda ya Dodoma na Tanga mitambo hiyo itazimwa Januari 30, 2013. Maeneo husika yakiwa ni Manispaa ya Dodoma Kibaigwa, Mvumi Mtera na Mkinga likiwa eneo la kumalizia. Vituo vitakavyohusika ni: TBCI, ITV, EATV, TV ya Manispaa ya Tanga na ATN.

Dkt. Mukungara alisema wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo hayakutajwa katika ratiba hiyo, wataendelea kupata matangazo kupitia mfumo wa matangazo ya televisheni kama ilivyo sasa hadi hapo mitambo ya kupokea mfumo wa matangazo ya dijitali itakapokamilika kwenye maeneo yao. Alizitaka kampuni zinazoweka mitambo ya dijitali kuongeza kasi ili kuhakikisha kuwa ujenzi wa mitambo hiyo unakamilika nchini kote kabla ya mwaka 2015.

Imetoholewa kutoka Hellen Mwango, *Nipashe* (2013)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU C**

## SAMAHANI YAWEZA KUONDOA KINYONGO NA KUOKOA UHUSIANO



Huwa inasemwa kuwa tenda wema nenda zako usingoje shukrani. Na kwamba binadamu ni kiumbe asiyekumbuka wala kujali wema. Ubinadamu huweza kuthibitishwa kwa vitu vidogo ambavyo wakati mwingine unaweza kuvidharau. Pia hakuna binadamu kamili, wote tuna udhaifu.

Kutokana na udhaifu tulio nao ndiyo maana wakati mwingine tunajikuta tunafanya au kusema mambo ambayo yanawaumiza wengine. Vitendo hivi vya kikatili huwa vinauma zaidi vinapotendwa na ndugu ama jamaa wa karibu kuliko vinapotendwa na mtu wa mbali.

Kuna jirani wangu ambaye yalimkuta haya ya kufadhili ndugu zake na hatimaye wakamtenda na kumdharau kama vile sio ndugu yao. Huyu kaka akanisimulia jinsi alivyojibebesha jukumu la kuwalea, kuwatunza na kuwasomesha ndugu zake hadi wakapata kazi na kujitegemea na wengine kufunga ndoa na kuanza maisha yao.

Huku akitikisa kichwa kwa huzuni akasimulia alivyoweka pembeni mambo yake mengi kimaisha ikiwemo kumaliza shahada yake ya kwanza ili apate kuwasomesha ndugu zake nao waweze kujitegemea.

Kawaida katika maisha kuna kupanda na kushuka na huyu kaka shughuli zake za kibiashara hazikumwendea vizuri. Akajikuta anaandamwa na madeni na huku asiwe na njia ya kudumu ya kumwingizia kipato. Hivyo akajaribu kutafuta jinsi ya kujisimamia tena kimaisha. Na katika shughuli zake akasafiri nje ya nchi kujaribu kuangalia uwezekano wa biashara. Ndiposa wakati akiwa kwenye harakati, ndugu zake wakafanya njama, wakaleta dalali wakasomba vitu vyote vya nyumbani na kwenda kuvipiga bei wakidai wanataka kulipa madeni yake.

Kwa kifupi ni kwamba wale aliowaita ndugu zake wamemsafisha na kumwacha mweupe bila chochote. Na hivi sasa anaanza tena maisha upya akijaribu kujitibu majeraha ya moyo wake. Hivyo nilipopata nafasi ya kuzungumza naye nilimsisitizia umuhimu wa kusamehe na kuweka huru roho yake. Nikamkumbusha kwamba waliompora mali zake hawajampora nguvu, akili na uwezo wa kutafuta mali nyingine zaidi ya zile alizokuwa nazo.

Unaposamehe unajipunguzia ***[ – X – ]*** ambayo umeyapata kwa uliyotendewa. Kawaida watu wanapokutenda na kukufanyia ukatili wanakuwa **[ – 27 – ]** sana kuomba **[ – 28 – ]** wakidhani kwa kufanya hivyo watakuwa wamejishusha sana. Hawataki kuonekana kuwa ni **[ – 29 – ]** na kukubali **[ – 30 – ]** walio nao kwa kuomba msamaha.

Imetoholewa kutoka Sizarina, *Taifa Leo* (2013)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU D**

# JANUARI YAANZA NA IDADI NDOGO YA WATALII PWANI

**Mombasa na Mathias Ringa**

Hoteli za pwani zimekumbwa na upungufu mkubwa wa watalii baada ya msimu wa Krismasi na Mwaka Mpya kuisha. Wakati wa Krismasi na Mwaka Mpya, hoteli katika mji wa Mombasa, Malindi, Watamu na Diani zilijaa kutokana na idadi kubwa ya watalii kutoka humu nchini.

Baadhi ya hoteli za Mombasa zilikuwa na asilimia 80 ya watalii kutoka humu nchini wakati wa msimu wa sherehe. Lakini baada ya msimu wa sherehe kuisha, hoteli za Mombasa na Lamu zina wageni wachache mno baada ya watalii kutoka humu nchini kurudi kazini na wanafunzi kurudi shuleni.



Kulingana na Mwenyekiti wa Chama cha Utalii, Mombasa na Pwani (MCTA) Bw. Mohammed Hersi, hoteli nyingi za Mombasa zina asilimia 40 ya wageni.

**Ugaidi**

Kati yao, alisema, ni watalii kutoka nchi za nje na wageni ambao wanahudhuria mikutano na warsha. Bw. Hersi alituarifu kuwa idadi ya watalii kutoka Ulaya ni ndogo kwa sababu ya tisho la ugaidi na kuzoroteka kwa uchumi barani Ulaya.

"Baada ya msimu wa sherehe kuisha, hoteli nyingi za Mombasa zina wageni wachache mno kutokana na wageni wa humu nchini kurudi kazini na vile vile shule kufunguliwa", akasema.

"Kwa sasa hoteli zinategemea maandalizi ya mikutano na warsha na watalii wachache kutoka mataifa ya kigeni", akaarifu. Hata hivyo, Bw. Hersi alisema kuwa hoteli za Lamu ndizo ambazo zinakumbwa na uhaba mkubwa wa watalii. Bw. Hersi ambaye pia ni Afisa Mkuu wa Hoteli za Heritage aliarifu kuwa hoteli katika Kaunti ya Lamu zina asilimia 20 ya wageni kutokana na athari ya visa vya ugaidi vilivyotokea miaka ya hivi majuzi.

Mkuu wa Utalii katika Kaunti ya Kwale, Bw. Adam Sheikh, alisema kuwa hoteli za Pwani Kusini zina asilimia 60 ya wageni baada ya msimu wa sherehe kuisha.



https://xtremepape.rs/

**Ughaibuni**

Bw. Sheikh alidokeza kuwa idadi kubwa ya wageni ni watalii kutoka Ujerumani, Uingereza, Italia, Ufaransa na Australia. Hoteli za Pwani Kusini, alisema, zitaendelea kupokea watalii kutoka Ulaya hadi Machi mwaka huu.

"Ijapo idadi ya watalii kutoka humu nchini imeshuka mno, bado tuko na watalii kutoka Ulaya ambao wataendelea kuwasili hadi Machi." Ili kuimarisha sekta ya utalii nchini, Bw. Sheikh aliomba serikali kuu kuruhusu mashirika zaidi ya ndege ya kimataifa kuanzisha safari za moja kwa moja kutoka Ulaya hadi Mombasa.

Afisa Mkuu wa Chama cha Kutoa Huduma za Hoteli Nchini (KAHC) tawi la Pwani Bw. Sam Ikwaye alisema kuwa hoteli za Malindi na Watamu zina kati ya asilimia 50 na 60 ya wageni kutokana na watalii kutoka Italia.

Imetoholewa kutoka Mathias Ringa, *Taifa Leo* (2014)



https://xtremepape.rs/